# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Unguja*
*13 Agosti, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

### RAIS SAMIA AZINDUA MRADI WA MAJI KIZIMKAZI, ASISITIZA AMANI, ULINZI WA MIUNDOMBINU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tarehe 13 Agosti, 2026, amezindua Mradi wa Maji Kizimkazi na kuwataka wananchi kulinda na kutunza miundombinu ya maendeleo inayowekezwa katika eneo hilo.

Akizungumza na wananchi baada ya uzinduzi, Rais Dkt. Samia amesema mradi huo na miradi mingine ya maendeleo imeigharimu Serikali rasilimali nyingi, hivyo ni muhimu ilindwe ili iendelee kutoa huduma kwa muda mrefu.

*"Ndugu zangu, sambamba na hatua zote tunazoendelea kuzifanya, niwaombe sana kuipenda, kuilinda na kuitunza miundombinu hii,"* amesema Rais Dkt. Samia.

Rais Dkt. Samia amesema uwekezaji katika miundombinu ya maji Kizimkazi umezingatia mahitaji ya sasa, pamoja na ongezeko la idadi ya watu na shughuli za kiuchumi katika eneo hilo.

Mradi huo umejumuisha uboreshaji wa chanzo cha maji cha Machomwe, ujenzi wa tangi jipya la lita milioni moja, mfumo wa kutibu maji na pampu zenye uwezo wa kusukuma **lita 100,000** kwa saa, zinazoendeshwa kwa nishati ya umeme na jua.

Maboresho hayo yameongeza uwezo wa kuhifadhi maji kutoka **lita 150,000** hadi **lita milioni 1.15**, huku hatua inayofuata ikiwa kuimarisha usambazaji ili huduma iwafikie wananchi katika maeneo yote yanayolengwa.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema miundombinu inayotekelezwa Kizimkazi ina mchango wa moja kwa moja katika maisha, uchumi na ustawi wa wananchi wa eneo hilo na maeneo mengine.



*Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

Katika hatua nyingine, amesisitiza umuhimu wa kuendelea kulinda amani na utulivu, akisema mazingira hayo ndiyo yanayowezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

***"Miradi hii ni uhai wetu, ni fursa zetu, ni uchumi wetu na ustawi wa maisha yetu,"*** amesema Rais Dkt. Samia.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso, amesema maboresho yaliyofanyika yameipa Kizimkazi uwezo wa kupata takribani **lita milioni 2.4** za maji, dhidi ya mahitaji ya sasa ya takribani **lita 500,000**.

Amesema ongezeko hilo linaimarisha uhakika wa huduma kwa wananchi na kuweka mazingira yanayoweza kuhimili ukuaji wa shughuli za uwekezaji katika eneo hilo.

Waziri Aweso amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia inaendelea kupanua huduma za maji vijijini Tanzania Bara, huku ikilenga kufikisha huduma katika vijiji vilivyosalia ndani ya miaka mitano.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Seif Kombo Pandu, amesema mradi huo unaakisi ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Amesema wizara za maji za pande zote mbili zimeendelea kushirikiana katika utekelezaji wa miradi na sasa zinaendelea kupanua ushirikiano huo kupitia kubadilishana wataalamu na uzoefu katika uendeshaji wa sekta hiyo.

Mapema leo, Rais Dkt. Samia alitembelea Kituo cha Afya Kizimkazi, ambako alipanda mti, kushuhudia makabidhiano ya gari la wagonjwa na kukagua huduma za matibabu ya kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo.

Rais Dkt. Samia amesema kituo hicho kinaendelea kupanua huduma zake, ikiwemo mpango wa kuongeza tiba kwa mazoezi ya viungo kwa majeruhi wa michezo na watoto wanaohitaji huduma hiyo.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia alitembelea chanzo cha maji cha Machomwe na Skuli ya Mafunzo ya Amali, Mkunguni, Kizimkazi, ambako aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa skuli hiyo.

Shughuli hizo ni mwendelezo wa ratiba za Rais Dkt. Samia kuelekea kilele cha Tamasha la Kizimkazi mwaka 2026.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu